# Methali za Kiswahili katika Kukabiliana na Ufisadi Nchini Kenya

*Joseph Nyehita Maitaria*
*Chuo Kikuu cha Karatina, Kenya*

**Ikisiri**

**Kero za ufisadi (kwa sasa) zimekuwa zikigonga vichwa vya habari katika vyombo vya habari na kuzungumziwa kila uchao nchini Kenya. Visa hivyo vimezagaa na vingali vinarindima katika maisha ya watu. Wananchi wanaonyesha dalili za kusinywa na vitendo hivyo na wamekuwa wakiitaka serikali kutoa adhabu kali zaidi kwa wote wanaoendeleza visa hivyo. Suala hili limekuwa likiwapiga ngeo wananchi; wanaposhuhudia wale wanaonaswa au kuhusishwa katika vitendo hivyo; hufikishwa mahakamani na kutokea milango wa nyuma. Hili si jambo la mzaha; inaashiria kuwa, matumizi ya nguvu hayajafua dafu na hazijawa mwafaka kama njia ya kukabiliana na janga la ufisadi. Athari ya ufisadi nchini Kenya zi tele; mshikamano wa watu unaendelea kumomonyoka, akina yakhe nao hawana cha kutumaini wala kutegemea na wanaendelea kumasikinishwa; nazo fedha za umma zinazotokana na ushuru zinaendelea kupotea pote! Makala haya yanajaribu kuelezea namna methali za Kiswahili zinavyobainisha sura mbalimbali za ufisadi kwa azma ya kuwaongoza wanajamii katika kujenga mikakati ya kukabiliana na janga hilo nchini Kenya kwa wakati wa sasa.**

**Maneno Muhimu:** Methali za Kiswahili; Ufisadi, Athari

## Utangulizi

Ufisadi ni jinamizi linaloitambalia na kuiguguna mihimili muhimu ya maendeleo katika mataifa mengi duniani na Kenya ikiwemo; si kero inayoshuhudiwa katika taifa moja tu. Taifa la Kenya wakati wa sasa linakatishiwa ndoto iliyokuwepo na matumaini ya wale waliopigania uhuru kutoka kwa watawala wa ukoloni. Hivyo, ili kufahamu yanayoshudiwa wakati wa sasa, unahitaji kufahamu historia ya jamii inayozingatiwa. Wananchi, hasa katika mkesha wa uhuru (katika miaka ya 1960 na katika mwongo wa kwanza baada ya uhuru) walikuwa na maazimio kidedea ambayo yalikuwa bayana: kuondoa ukabila, kukabiliana na maradhi na ujinga. Aidha ieleweke kuwa, '*Kujenga ni kugumu, kubomoa ni rahisi'*. Masuala haya yanawiana katika kuujenga na kuuimarisha uchumi wa nchi kwa kuwashirikisha wanajamii.

Misururu ya sakata za ufisadi imekithiri na jua halizami bila ya sauti za kusikitisha na kukirihisha masikio ya Wakenya. Ingawa nchi ya Kenya haijapungukiwa kwa rasilimali, imekuwa kama chombo kinachoyumba kwenye bahari kutokana na ufisadi uliokithiri katika jamii. Hivi sasa, ni zaidi ya miongo mitano na nusu baada ya uhuru na visa vya ufisadi vinaendelea kulifukarisha na kulichafua jina la taifa (Tazama taarifa ya Shirika la habari la Marekani la PBS tarehe 11 April, 2016 na kunukuliwa na B.M.J. Murithi na Wanderi Kamau katika gazeti la *Taifa Leo* la tarehe 14 Aprili, 2016 uk. 3 kuwa, 'Ufisadi Kenya waangaziwa kimataifa' ambapo inasemekana kuwa, 'Kenya sasa yatambuliwa kama, Ngome ya Hongo'). Hali hii inahofisha na kulipaka tope taifa la Kenya katika ngazi za kimataifa. Kutokana na ufisadi, taifa hili limeshuhudia miaka ya giza na hatua za maendeleo zina nyufa pana. Baadhi ya wale walioweza 'kunufaika' na ufisadi wamekwa fidhuli na wanafiki na wanajipiga kifua kuwa, hizo ni 'jitihada' au 'juhudi' zao za 'kujichumia' na 'kufurahia matunda ya uhuru'. Wanasema kuwa 'wanajijengea ngome ya maisha ya kesho' huku wakijichukulia kuwa wao ni 'mashujaa'. Hawajali wala hawapigwi mshipa kwa sababu ya vilio vya ndani kwa ndani vya walio wengi katika taifa hili (Maitaria, 2014b). Sababu hapa ni, *'Mwenye shibe hamjui mwenye njaa'*. Aghalabu, watu hao hujiliwaza kimoyomoyo: 'Watanitambua mimi ni nani katika taifa hili?' na 'Hawa wanachokoza nyuki na wawe tayari kuumwa'. Isitoshe, wanapoelekezwa kidole cha lawana au tuhuma zinapoelekezwa kwao; huzua sarakasi kwamba, wanasimangwa, wanaonewa gere kwa utajiri uliotokana na 'jasho lao' na uluwa walio nao. Angalia kauli za baadhi ya vigogo wa kisiasa na viongozi wanavyolumbana pindi wanapotuhumiwa, "Siwezi kujiuzulu kwa sababu ya kutajwa … kuhusiana na kashfa ya wizi wa pesa za …. Nilihusika vipi na ufisadi? Nilipata faida gani? ... Alimtaka … akome kuzungumzia suala la ufisadi akidai yeye pia ana washirika ambao wamehusishwa na sakata za ufisadi nchini. Historia ya … imegubikwa na madai ya ufisadi na pia ni rafiki wa karibu wa watu wanaohusishwa na sakata kubwa za ufisadi nchini … ni … mshirika wa … wanaohusishwa na … wa ulanguzi wa dawa za kulevya … Alitaka … kujua ni kwa nini … amekaa kimya kuhusu ufisadi zinazokumba …mahakama." (Leonard Onyango ambaye aliripoti hayo kwenye gazeti la *Taifa Leo* la tarehe 29 Februari 2016, kur. 1-2.) Watu wa sampuli hii, wanalijali na kujivunia taifa lao? Kwa kawaida, lisemwalo hadharani, silo. Kauli zao zinaelekezwa zaidi na masuala yanayohusu tumbo. Wanasahau kuwa *'Mugwana ni vitendo'* na wala hakuna lenye mizani ya kujisifia. Mahakama zipo na wanaposukumwa kizimbani, huwa wajanja na wanajua kuicheza ngoma. Mawakili wenye uchu wa kusimamia kesi hizo wapo na wamehitimu na wanaimaizi taaluma yao; wako tayari kwa makali yanayoshamiri hila na ujanja katika kuwatetea wateja wao kufa kupona.

**Mwelekeo wa Watu kuhusu Ufisadi**

Mwelekeo wa malumbano miongoni mwa watuhumiwa wa ufisadi nchini Kenya (kama ilivyobainishwa hapo awali) unawafanya wananchi kutilia shaka utaratibu mzima wa utendaji haki kutokana na madai ya ufisadi kwa 'kupangusana jasho' kwa hila na 'kunawishana mikono' katika taasisi za mahakama. Malengo yanayowaelekeza

kufanya hivyo ni, kugawana 'ngawira' nono hata kama kithibiti kipo kama inavyoashiriwa katika methali *'Mkamatwa na ngozi, ndiye mwizi'*. Kihalisia ni kwamba, *'Mchelea haki hasemi ukweli'*. Matokeo ni kwamba, watu hao hawawezi kutenda lililo la haki na kila wakati huibatili haki katika jamii kwa manufaa ya kibinafsi. Siku mbili-tatu wateja hao wameachiliwa huru, wakishindana zaidi katika kugombea uongozi wa maeneo-bunge wanakotoka. Huko, wanachukuliwa kuwa ni 'wana wa kisasa waliojitahidi' na 'kurudi kwao'. Baadaye, wanatarajiwa kuwa mstari wa mbele katika kuwashika Wakenya mkono na kuwaonyesha njia ya kuututumua na kuuimarisha uchumi wa jamii! Katika baadhi ya maeneo hayo, watu hawaulizi ubwanyenye huo alioupata kwa muda mfupi umetokana na harakati gani au ni sakata ngapi alizohusishwa nazo! Kwani, kunani? Hawa ni 'walinzi' na viongozi wastahiki katika jamii au wanaolinda himaya zao! Isitoshe, wao huchukuliwa kuwa wajuzi wa mkondo wa maendeleo katika nchi kwa mabunda ya fedha zinazomwagwa katika maeneo watokako. Matokeo ni kwamba, huwanyima wananchi (ambao ni wapiga kura) haki ya kumchagua kiongozi mstahiki wanayempenda kwa njia iliyo wazi. Wanapokuwa katika vikao vya bunge, wao huwa vizingiti vya miswada yenye tija kwa taifa. Wahusika hao[1] ni mifano hai ya viongozi bandia wanaojitakia makuu ya uwekezaji kwa njia batili za mkato ambazo zinazohujumu demokrasia na haki ya wananchi. Kinachovunja mioyo ya watu ni kuwa, pepo hizo za ufisadi zimekuwa zikinyemelea baadhi ya sekta na asasi muhimu nchini Kenya (hata mahakama zilizopo!). Hivyo, linapaswa kuangamizwa na kufifishwa katika jamii. Njia za mkato za kujinufaisha kiulaghai zimekuwa zimekithiri na hazina mafao yoyote kwa taifa hili.

Wale wafisadi wanaowekewa mitego na wasioweza kujinasua hujipata wakijikanganya kwa mibwabwajo sauti za kutisha na maneno yasiyoeleweka. Kauli kama vile 'si mimi' au 'si kuwa peke yangu' na 'naomba samahani!' Sauti hizi zinachukiza na kusikitisha kila uchao. Swali hapa ni je, watu hawa wanajihusisha na visa vya ufisadi kwa kufahamu au kutofahamu madhara yake katika jamii? Jibu hapa ni kwamba, wana ufahamu tosha kuwa, huu ni *'mwiba wa kujidunga'* ambao *'hauna maombolezi'*. Zaidi ya kuwa wahalifu, mahasidi katika jamii, wamekuwa kikwazo kikuu kwa taifa la Kenya, adhabu na hatua kali za kinidhamu zimekuwa zikitumiwa lakini bado vituko hivyo. Hayo hayajasitishwa na yanaendelea kutendeka kupitia kwa sura mbalimbali. Ingawa ufisadi umekithiri na unayumbisha uchumi wa nchi na kulipaka tope taifa hili, ni muhimu kuupiga vita. Hata hivyo, ni muhimu kueleweka kuwa, '*Moto hauzimwi kwa moto'*. Kuna haja ya subira katika kuelekezana, kuonyana na kufahamishana kupitia kwa kauli mbiu zilizopo katika jamii kuhusu mwafaka unaotarajiwa. Miongoni mwa kauli hizo ni unuwai wa methali za Kiswahili zilizopo ili

[1]Watuhumiwa katika masuala ya ufisadi hawakutajwa katika makala haya kwa sababu ya heshima. Pindi inapohitajika, majina yao yanaweza kupatikana katika baadhi ya vyombo vya habari vilivyopo nchini Kenya.

zitumiwe kuwasilisha jumbe za heri njema na kujenga msingi wa tafakuri na uhakika kwa kuelekezana kuhusu maingiliano ya watu kwa kuzingatia utamaduni wa jamii (Maitaria, 2014a; Abou-Zaid, 2013; Kalugila na Lodhi, 1980). Kwa sababu methali za Kiswahili zinatokana na utamaduni wa wenyeji wa Afrika, zimekuwa zikitumiwa tangu jadi katika kuonya, kutafakari, kukosoa, kukumbusha, kutanabahisha na kuiadilisha jamii. Methali ni ishara zinazoweza kufasiriwa kwa kuzingatia hali halisi katika jamii (Nsokwa, 2011; Wanjohi, 1997). Kwa ujumla, methali za Kiswahili zinaweza kutumiwa katika kubainishia uhalisi wa maisha ya watu na kutoa mwelekeo kuhusu namna ya kukabiliana na masuala ambayo yanahatarisha ushikamano wa jamii kama vile ufisadi katika taifa la Kenya. Makala haya yanangazia baadhi ya methali hizo kwa malengo ya kubainishia tathmini-elekezi zinazoweza kutumiwa katika kukabiliana na ufisadi katika jamii ya sasa nchini Kenya. Janga hili la ufisadi linajitokeza katika viwango viwili: cha mtu binafsi na umma kama itakavyobainishwa hivi punde.

**Chanzo cha Ufisadi katika Jamii**

Ufisadi huhujumu uchumi na kusambaratisha jitihada za watu katika maendeleo. Ni katika hatua hii ambapo inaweza kuhojiwa kuwa: uzalendo wa baaadhi ya Wakenya ni wa kiwango gani; upo au umefikia wapi katika jamii ya sasa? Kuna ngazi mbili katika ubainishaji wa chanzo cha ufisadi: ya kitaifa (kijamii) na kibinafsi.

**Ufisadi katika Ngazi ya Kitaifa**

Sehemu hii itabainisha namna sura za ufisadi unavyojishaua katika ngazi ya kitaifa au umma. Zimwi la ufisadi limekuwa wingu zito ambalo limetanda na linakatisha juhudi muhimu za wananchi kuhusu maisha yao na uchumi wa taifa. Sura hizo ni kama zifuatazo:

i. Ubinafsishaji wa baadhi ya miradi ya umma. Kutokana na msukumo wa tamaa, baadhi ya watu wenye nyadhifa za juu wamekuwa mbioni katika kuhodhi rasilimali na miradi muhimu inayoanzishwa na serikali kwa manufaa ya jamii. Baadhi yao hutumia ujanja kuzivuta baadhi ya rasilimali zilizopo kwa manufaa ya kibinafsi ilihali wanasingizia misukumo ya nguvu kutoka nje ya nchi. Methali za '*Mvunja nchi ni mwananchi*' na '*Kikulacho ki nguoni mwako*' ni baadhi ya kauli zinazotoa taswira ya hali halisi iliyopo katika jamii na vilevile kuwataka wanajamii kuwa macho na kujihusisha kwa dhati katika harakati za kuwasaka wafisadi ambao ni 'madoadoa' miongoni mwa wana wa nchi wanaocheza ovyo ndani ya nchi na wala si wana wa nje ya nchi. Kadhalika, wafisadi huwa mafundi wa uongo na zaidi, wale wa ngazi za juu katika taifa huwa wanatumia 'nguvu' au 'makali' ya kalamu katika kuhamisha kitita cha fedha za umma na kubatilisha haki. Haya yanaendeleza zaidi visa vya ufisadi na si kwa kitu kidogo bali kitu kikubwa. Watu kama hao wapo na wamejificha katika jamii. Kijuujuu, wao huonekana kuwa wastahiki wa kutegemewa, kumbe wana 'madoadoa' yanayouhujumu zaidi uchumi wa taifa la Kenya na kuathiri mno mihimili mikuu ya maisha ya watu wa kawaida. Aghalabu, ufisadi unaendelezwa na hao vigogo katika jamii na la kuhuzunisha

ni kwamba wanaosingiziwa ni wale wadogo wanaowategemea'wakuu' hao. Hili linadokezwa kwa methali, *'Akosapo mkubwa, mdogo huadhibiwa'.* Watakaowatetea hawa akina yakhe ni kina nani, isipokuwa Mungu! Matokeo ya vitendo hivi, ni kusaliti na kulemaza juhudi za wanajamii katika maendeleo ya taifa lao (Maitaria, 2018). Tamaa ya kujitajirisha kwa haraka huwaelekeza baadhi ya watu kuhiari hujiingiza katika vituko vya utoaji na upokeaji wa milungula. Kimsingi, mizungu inayoendelezwa katika ufisadi ni ya kuwili: anayetoa na anayepokea rushwa. Kwa mfano, mtu akienda polisi kutoa maelezo kuhusu namna alivyotoa hongo au pesa; aghalabu huachwa huru na anayepata 'hatiani' ni yule mtoaji ambapo sivyo. Hata yule anayepokea ana hatia.

ii. Suala la siasa katika taifa. Aghalabu ufisadi, huhusishwa na masuala ya siasa katika nchi ya Kenya. Badala ya kuwashajiisha wananchi katika mwafaka huo; uhusika wa baadhi ya watu ni wa 'kutarajia' na wala si kuchangia mawazo moja kwa moja. Hivyo, suala zima la demokrasia katika taifa linaborongwa kwa kupewa sura nyingine inayojikita kwenye uchu wa tamaa ya kujitajirisha kwa haraka. Baadhi ya watu hapo awali walichukuliwa kuwa 'waheshimiwa' kutokana na misimamo yao ya utu na kujali masilahi ya watu katika jamii. Kutokana na misimmo yao, walipata mwanya wa kujihusisha na siasa na hatimaye kuwania nyadhifa kuwakilisha maeneo-bunge yao huku wakielewa fika kuwa wanajali masazo ya matumbo yao. Ukweli ni kwamba hawa huwa mawindoni ili kupoza mchecheto wa uchu wa kujitajirisha kwa haraka na wala si msukumo wa kulitumikia taifa lao. Aidha, fedha zinazopatikana kwa haraka wanapokuwa wameshikilia nyadhifa za juu serikalini hutumiwa chapuchapu kama chambo au kivutio cha 'kulainisha nyoyo' za wapiga kura kwa malengo ya kugeuza mielekeo na misimamo yao ya kisiasa. Methali ya *'Maji ambayo hukujitekea hayatulizi kiu'* inawaelekeza wale ambao huyumbishwa kwa fedha za kuwahonga huwa kichele na haziwezi kuwa tegemeo katika maisha. Ujumbe unaowasilishwa katika methali, *'Kinachopatikana kwa haraka, hupotea kwa haraka'* ni kwamba, fedha zinazopatikana kwa hila; hufujwa katika mambo yasiyokuwa ya muhimu, yanayolenga ujilimbikiziaji wa sifa, anasa na starehe. Wanapokuwa wamefanikiwa katika mradi wao; watu wa kuwapa hongera wapo na hata wale waliowatia mbaroni hapo awali wapo katika kundi lilo hilo. Mbinu kama hizi zilizojaa hila huwa na athari ya kuwafanya wananchi kuwapigia kura viongozi wasiofaa. Kuingia bungeni huwa kama tiketi ya kujinufaisha badala ya kuwahudumia wananchi waliomchagua. Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini Kenya (IEBC) imekuwa ikiwahimiza wananchi kutathmini sera za wawaniaji ubunge katika maeneo yao na katu wasipotoshwe na kuelekezwa na rushwa. Ushauri huo huwa unasahaulika fedha zinapomwagwa na matokeo yanapotangazwa huwa 'wamenunuliwa'. Huu ni *'Msiba wa kujitakia* na *hauna maombolezi'.* Mwelekeo huu ni utamaduni mbaya unaobeua na kuutia doa mstakabali mzima wa suala la uongozi katika taifa hili.

iii. Huduma kwa umma. Kutokana na tamaa ya fedha zaidi ya mshahara halali katika vituo vya kutoa hudumia kwa umma, baadhi ya watumishi wa umma hujihusisha na visa vya ufisadi ambapo watu au 'wateja' hupata huduma kwa misingi ya 'mwenye nacho'. Kutokana na kawaida hizo, baadhi ya vituo hivyo huwa vya 'kuwanawisha mikono', kuingiwa kiwi machoni na upokeaji rushwa huku 'wanaozawadiwa' wakiwa watu wa ukuruba nao. Bila soni, wao huwaambia wanaotaka huduma kuwa, *'Mkono mtupu haulambwi'*. Hati halali hubatilishwa kwa kalamu. Hivyo, watu raia wanaotarajia kupata huduma hutapeliwa. Kwa mfano, katika ununuaji wa mashamba kihalali maaafisa ambao huhitajika kuwahudua watu, katu hawaamki vitini kutoa hudumia bila ya mikono yao 'kupakwa mafuta'. Utapeli huo huanzia katika afisi za ardhi ambapo maafisa hao hushirikiana na mawakala ambao hutoa habari mbadala kuhusu vipande hivyo. Matokeo huwa hati halisi kubatilishwa na wateja kuuziwa ardhi kwa hati ghushi. Kadhalika, taasisi hizo za umma zimezorota na dawa hazipatikani au zinapotolewa huwa zisizofaa ila kwa kuingia mfukoni kutoa chochote.

iv. Visa vya udanganyifu au kutozingatia ukweli. Ujenzi wa majengo ya ghorofa umeingia matatizo mengi ambapo wanaohusishwa katika kandarasi hizo, hutumia ulaghai na njia za mkato. Mfano ni jengo la ghorofa nne katika mtaa wa Zimmerman Nairobi ambalo lilitiliwa shaka miaka miwili kabla ya kuporomomoka[2]. Kadhalika, visa vya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa vimekuwa vikishuhudiwa na vilikithiri mno katika mtihani wa kitaifa mwaka wa 2015 hata ingawa ulinzi mkali ulikuwepo. Ukweli ni kwamba, watahiniwa ambao wana umri mdogo hawatarajiwi kuwa ndio walioipata mitihani hiyo bali inatokana na mitandao ya kichinichini inayohusisha baadhi ya maafisa wafisadi wa Baraza la Mitihani ya Kitaifa (KNEC) ambao wako tayari 'kuupinda mkono' na baadhi ya wazazi ambao wako tayari 'kunyoosha mkono'. Huenda ni idadi ndogo tu ambayo hutiwa mbaroni lakini wanaoathirika ni wanafunzi wasiokuwa na hatia. Tahadhari hapa inatolewa kupitia kwa methali, *'Majuto ni mjukuu, mwisho huja kinyume'*; *'Mchelea haki hatendi ukweli'* na *'Tamaa mbele mauti nyuma'*.

v. Kutokuwajibika na utepetevu kazini: Kuzembea kazini; kufika wamechelewa na kutoka kabla ya wakati au kutofika kazini na kutoa sababu zisizokuwa na msingi. Aidha, wanalaza damu katika kazi za utumishi kwa umma na kazi za kando ndizo zinazopewa kipaumbele. Matumizi mabaya ya fedha pasi na kujali hali ya uchumi katika nchi. Mfano ni katika matumizi yasiyo ya vifaa

[2]Hiyo ni taarifa ya Aggrey Mutuambo, Samuel Karanja na Valentine Obara katika gazeti la Taifa Leo la tarehe 10 Machi, 2016:2).

vya umma au serikali na matumizi magari ya serikali kwa shughuli za kibinafsi.

vi. Ukiukaji wa sheria na katiba ya nchi. Wanaopatikana na hatia za ufisadi hupewa adhadbu yenye unafuu. Wanafahamu namna ya kuuzunguka mbuyu na matokeo ni kwamba, sheria zinabatilishwa, hupindwa na huwapendelea zaidi walalahai 'walionacho' na walalahoi hawapewi halali yao. Nchi imekuwa ni ya wale walio na mali au utajiri unaotiliwa mashaka na hakuna cha mno kinachoendelea.

**Ufisadi katika Ngazi ya Kibinafsi na Kijamii**

Ufisadi ni jambo ambalo linaendelezwa na watu wa matabaka mbalimbali na linashuhudiwa kila uchao. Baadhi ya mambo ambayo yanakuwa kama kichocheo cha kujiingiza katika vitendo vya ufisadi ni kama yafuatayo:

i. Haja ya kuikidhi mahitaji muhimu ya familia. Kushindwa kupata mahitaji ya lazima katika maisha huweza kuwa fursa au chemichemi ya kujiingiza katika masuala ya udanganyifu na kunyemelea mali ya wengine. Ingawa vitendo hivyo vinakemewa katika jamii, baadhi ya watu huweza kuchukulia (bila kujua) kuwa ni harakati ya kawaida maishani.

ii. Tamaa na kujitakia makuu. Hii kiu ya kujitakia makuu huwaelekeza baadhi ya watu katika visa vya uhalifu kama vile ufisadi na ujambazi. Ushauri unaopasa kuelekeza maisha ya watu ni ule wa *'Mwenye choyo hashibi'* na kwamba kuridhika ni muhimu kama inavoelezwa kwa methali: '*Mtu hujikuna ajipatapo*'. Baadhi ya watu wamekuwa na msongo wa mawazo kwa kuamini kuwa 'bila pesa maisha hayaendi'. Kujitakia makuu husababisha kutokuwepo na amani katika jamii**.** Huu ni upofu unaoelekezwa na hali ya kuabudu zaidi fedha. Vitendo vya ufisadi vinafedhehesha na vinalichafua jina la mhusika hata baadaye kwa sababu '*Mla samaki haachi kunuka shombo'* na tahadhari hutolewa kimbele kupitia kwa methali kwamba, *'Tamaa mbele mauti nyuma'.* Jamii nayo huathirika kutokana na sifa zisizofaa za mmoja wao kutokana na sababu kwamba *'Samaki mmoja akioza ni mtungo mzima'* na *'Mchuma janga, hula na wa kwao'.* Ujumbe unaowasilishwa hapa ni kwamba, yeyote anayejiletea shida, huwatia hasara watu wa nasaba yake na jamii kwa ujumla. Kimsingi, anayestahiki kuelekezwa kidole cha lawama ni mhusika lakini pia taifa na jamii hupata pigo kutokana na vitendo vya mmoja wao.

iii. Ushindani katika jamii. Watu huogopa kushindwa hasa wanapojilinganisha na wenzao katika jaimii. Katika mazingira hayo ya kujidharau, dhana ya kuoneana wivu hujengwa katika bongo za wahusika. Athari ya mwelekeo huo ni kutumia njia za mkato, kutotumia haki na kuutukanisha utu wa mtu katika jamii na hii ndiyo sababu *'Chanda chema huvishwa pete'*. Katika muktadha huu, nchini Kenya kuna baadhi watu wastahiki ambao hawajiingizi katika matendo ya ufisadi na hao wanapaswa kutambuliwa. Kwa hivyo, samaki mmoja akioza si wote waliooza. Hawa wanahimizwa kuudumisha utu wao.

**Dhima ya Methali za Kiswahili**

Methali za Kiswahili zina ukwasi wa kushughulikia takribani kila kipengele cha maisha ya watu katika jamii. Kutokana na namna ujumbe unavyowasilishwa, methali zinazohusu masuala ya ufisadi katika kiwango cha mtu binafsi na taifa zinaweza kuainishwa kama ifuatavyo:

i. Methali za maelekezo, kurai au kutahadharisha. Mifano ni *'Mchuma janga, hula na wa kwao'*, *'Akiruka, usiruke naye, mtego utamsa';'Samaki mmoja akioza ni mtungo mzima'* na *'Tamaa mbele mauti nyuma'*. Hizi ni methali ambazo hujenga taswira ya hali ilivyo katika jamii.

ii. Methali za masharti na tahadhari. Kauli hizi ni za maelekezo ya kuzingatiwa kutokana na tajiriba ya wanajamii. Mifano ni, *'Usipoziba ufa utajenga ukuta'* na *'Kikulacho kinguoni mwako'*. Hizi ni methali ambazo zina malengo ya kuitahadharisha jamii kuhusu namna ya kuepuka na hali ya utepetevua au kutozingatia yale yanayotarajiwa katika uhalishi wa maisha ya watu.

iii. Methali za kukejeli. Hubeza baadhi ya vitendo ambavyo havifai katika jamii. Mifano ni *'Mwenye choyo hashibi'* na *'Tamaa mbele mauti nyuma'*. Hizi ni methali ambazo zinabeua au haziutukuzi ule unaoonekana. Malengo hapa ni kuwaonya watu kutojiingiza katika masuala ambayo yanaweza kuwaharibia jina au kuwavunjia heshima.

iv. Methali za sitiari. Humtarajia anayelengwa kupiga bongo zaidi ili kufikia maamuzi yenye mashiko kama vile: *'Nyani haoni kundule, mkono mtupu haulambwi'; 'Hakuna mchele ukosao ndume'* na *'Mkono ukishika mavi huoshwa'*. Baadhi ya matukio katika jamii huweza kufananishwa moja kwa moja na yale yanayopatikana katika maisha ya watu. Mfanisho huo si wa moja kwa moja lakini maana inayokusudiwa hupatikana kwa uelekezi wa tajriba ya watu katika jamii.

**Suluhu**

Janga la ufisadi limefisidi uchumi na kulipaka tope jina la taifa la Kenya. Hivyo, linahitaji kutafutiwa suluhu au 'dawa' ya dharura ili kulirejeshea sifa yake ya asili. Suluhu inahitaji kupitia kwa kauli za busara na hekima kama vile methali za Kiswahili zinazotokana na utamaduni wa wenyeji wa taifa hili na wala si kutoka nje. Suala la ufisadi linaweza kumulikwa kupitia kwa baadhi ya methali hizo. Inavyoelekea, uhalisi uliopo wa ufisadi katika jamii unayorejelewa ni kwamba, *'Hakuna mchele ukosao ndume'* na *'Mkono ukishika mavi huoshwa'* katu haukatwi! Huu ni ukweli mchungu unaotarajiwa kueleweka katika jamii na isitarajiwe kuwa watu wote katika taifa wameuvaa uzalendo. Shime ni *'Iwapo nia njia hupatikana'* kwa sababu, *'Aliyemfunza chui kula watu ni binadamu'*. Ingawa dosari hizo zinalemaza uchumi wa taifa, waliopotoka kwa kutofahamu (na hata wale wenye msimamo usiotetereka) wanahimizwa kuwa mfisadi *'Akiruka, usiruke naye; mtego utamsa'*. Kadhalika, jamii inahimizwa kwamba, *'Kuanza upya si ujinga'* na huo utakuwa mwanzo wa kusahihishana na kuelekezana kwa mtazamo mpya.

Kadhalika, *'Yaliyopita si ndwele, ganga (yaliyopo na) yajayo'*. Uelekezi unaotolewa hapa ni kwamba, yaliyopo au yaliyopita yanaweza kuangaziwa ili kuwa makini zaidi katika siku zijazo ili kosa lisirudiwe. Aidha, wito uo huo unawasilishwa kupitia kwa: *'Udongo uwahi uli maji'* na *'Moto huzimwa ukingali cheche'*. Linalorejelewa hapa ni kwamba, dharura ipo (ambapo ni dalili au ishara za ufisadi) na inahitaji kudhibitiwa inapochipuza; la sivyo taifa litajikuta katika hali ya kugharimika zaidi kuututumua na kuujenga uchumi wake. Hivyo kuna haja ya kuganga shina na kuing'oa mizizi yote ya ufisadi iliyojisimika katika taifa. Wakenya (kama jamii) wanahitaji kuwa na mwamko mpya na kujengewa mazingira ya matumaini kwamba, *'Mwizi siku zake ni arobaini'* au *'Siku za mwizi ni arobaini'*. Ni katika muktadha huu ambapo inawasilishwa kuwa, janga la ufisadi halitadumu milele; shime ni kila mtu kuamka kwa kuliwajibikia taifa lao. Isitoshe, methali hiyo ni onyo kwa wanaojihusisha na vitendo hivyo la sivyo wataimba wimbo kwamba *'Majuto ni mjukuu, mwisho huja kinyume'*. Isitoshe kuna msemo ambao umekuwa ukiendelezwa na baadhi ya wanajamii kwamba, 'Kenya haina wenyewe' bali ni stahiki ya kila mtu katika. Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi nchini Kenya (EACC) inahitaji kunoa makali zaidi ili kubainisha baadhi ya vitendo vya ufisadi vilivyofichika na wanaohusika wachukuliwe hatua na kuwa mfano kwa wengine wenye nia hiyo. Kuna haja ya hamasisho la dharura la jamii. Aidha, kuna haja ya kuwa na *'Hadhari kabla ya hatari'* na ni vyema kuwa macho, kujitambua na kuvirekebisha vitendo hivyo vinavyoendelea kujishauwa kila uchao badala ya kusubiri. Mazingira ya mwafaka huo yanaweza kupatikana kupitia kwa kauli za busara kama vile methali zipatikanazo kwa urahisi katika jamii.

Methali za Kiswahili ni kauli hai zinazoweza kutoa mwelekeo ufaao kwa kuzingatia miktadha ya matumizi yazo katika jamii (Mieder, 2008). Isitoshe, methali za Kiswahili ni kanzi ya ujumbe muhimu wa uelekezaji hasa zikilinganishwa na kauli za kijumla zinazotumika katika mazugumzo ya kawaida. Matumizi na maana yazo huweza kufasiriwa kwa namna mbalimbali (njia tofauti tofauti). Fasiri zinazotolewa kuhusu methali zinaweza kusadifu kwa kuzingatia muktadha wa matumizi, dhamira ya mtumiaji na uhusiano wa mtumiaji na hadhira yake (Babatunde na Mujidat, 2014). Hivyo, ni safari ndefu na ngumu inayohitaji juhudi za kila mja. Ufisadi umeleta madhara mengi ikiwemo kuwakatisha tamaa wazalendo wanaojituma katika kufanya kazi za halali. Kadhalika, vifo vinawakodolea macho baaadhi ya watu wasiokuwa na namna ila kutegemea huduma muhimu zinazotolewa katika taasisi za umma. Uporaji wa mali ya umma umekuwa wimbo tu. Ni wajibu wa kila Mkenya kuwa macho na kujihusisha katika harakati za kukabiliana na ufisadi kwa sababu vitendo hivyo vinahitaji kupigwa darubini na wanaohusika wanahitaji kuchukuliwa hatua na kuondolewa katika nyadhifa zao. Hii ndiyo nafasi ya kuirejeshea nchi hii ndoto na matamanio ambayo yaliaelekeza ndoto ya wazalendo waliopigania uhuru katika miaka ya mwishoni mwa 1950 na mwanzoni mwa 1960. Methali za Kiswahili zinaweza kutumiwa ili kulifanya taifa la Kenya kuwa la kutamaniwa na kuwa taifa la kujivunia na nyota barani Afrika. Matarajio ya Wakenya walio wengi ni kwamba, matawi hayatakatwa tu bali pia mizizi ya 'mti huu' wa ufisadi itang'olewa ili asilani isiweze tena kuchipuza katika taifa hili na hasa katika mioyo ya vikembe wa taifa hili.

Iwapo ufisadi utashamiri katika taifa hili la Kenya, vijana au vikembe hao (ambao kimsingi ni tegemeo la kesho) hawatakuwa wametayarishwa vilivyo katika kushika usukani wa kuliendesha taifa hili na muhimu zaidi, kukabiliana na maisha yao ya baadaye. Hivyo, watakuwa wamegubikwa pazia la giza la ufisadi hata bila ya ufahamu wao. Juhudi za kuwatayarisha viongozi hawa wa kesho zinahitaji kupaliliwa na kukuzwa wakati wa sasa wakiwa wangali wadogo la sivyo, hao watu wazima wataelekezwa kidole cha lawama kuwa *'Aliyemfunza chui kula watu ni binadamu'*. Ushauri unaotolewa hapa ni kuwa, '*Samaki mkunje angali mbichi'*. Vijana ambao watakuwa na mielekeo inayoashiria ufisadi wanaweza kuelekezwa la sivyo wataiga mwelekeo hasi uliojikita katika ufisadi ambao umekithiri kwa wakati wa sasa. Ndoto iliyokuwepo ya wapiganiaji uhuru itakuwa imezimwa na kufifishwa. Vijana hawatakuwa wenye maadili kutokana na kuiga mienendo na matendo ya wazazi wao au yale wanayoyaona (kwa wakati wa sasa) yakiendelezwa katika jamii. Tatizo kubwa kwa hivi sasa ni tofauti ya kimwelekeo baina ya wazee (ambao wanajali maslahi yao wenyewe) na vijana (ambao zaidi ya kuwa na mwelekeo wa kimaendeleo wanapuliziwa sumu ya ubinafsi na wazee wao). Hata hivyo, mwelekeo huu unaweza kuliharibia sifa taifa kwamba, *'Samaki mmoja akioza, ni mtungo mzima'*. Mwelekeo huo wa kimkumbo hauna mashiko na unabiuwa mwafaka miongoni mwa watu wanaojivunia kuwa Wakenya. Kauli hizo zenye kujumuisha lawama kwa wananchi zinaweza kufifishwa au kuzimwa kwa methali kwamba, *'Moto hauzai moto bali huzaa majivu'*. Aidha, vijana hawa wasipoelekezwa, 'wasipokunjwa' kama wangali wadogo; wanaweza kuwa tishio kwa amani na maendeleo ya taifa. Hivyo, kuna haja ya kuwatayarisha ili kuweza kushika hatamu katika kupambana au kukabiliana na sura mbalimbali za ufisadi zitakazokuwepo au pindi zitakapochipuza katika taifa lao. Jambo la fedheha ni watu katika taifa hili kuwa kama *'Pweza wa kujipalia mkaa'* kwa kuwapotosha baadhi vijana kwa kuwajengea dhana au mawazo kwamba, wanaweza kuishi maisha ya hawaa kwa kujipatia utajiri wa ghafla au ufanisi katika maisha kwa kujifanya wajanja au kuandama ulaghai unaojikita katika njia za mkato.

Isitoshe, mazingira yanayojengwa kupitia kwa methali hizo za Kiswahili ni kuwa, kuna haja ya kuwamulika wafisadi waliopo katika jamii na sura zote za ufisadi kwa kusema na kusikika; kusema kwa uwazi unaoweza kuthibitishwa; kusema ukweli wenye makali ingawa unaouma; kusema kwa uhamasishaji unaolenga kuwazindua watu ili kuweza kuuona uhalisi huo wa ufisadi. Ushauri huu unawasilishwa kwa methali *'Kusema kweli si tua'* na wale wanaoendekeza ufisadi wanataharishwa kuwa *'Lisemwalo lipo na kama halipolaja'*. Katika mazingira hayo, wananchi wanaweza kujengewa fikra endelevu na elekezi kwa malengo ya kumulika sura tatanishi zizongazo taifa hili. Aidha, wenye majukumu katika nyadhifa za juu serikalini wanahitaji kuwa katika mstari wa mbele kuukemea na kuwazindua wananchi kuhusu zimwi la ufisadi. Hili linawezekana, hasa wafanyapo ziara zao za mara kwa mara za kukutana na wananchi mashinani na mijini.

Methali za Kiswahili zinatadharisha kuhusu kuepukana na hali isiyofaa ya ushindani inayoelezwa kwa uchu wa tamaa. Kinachosisitiza wanajamii ni shime ya

kujituma kwa taifa lao na vilevile, kujitahidi katika kazi halali wazifanyazo na kuliwajibikia taifa lao. Nasaha hii inashadidiwa kupitia kwa methali zilizorejelewa hapo awali kama vile *'Mchuma janga, hula na wa kwao'* na *'Mvunja nchi ni mwananchi'*. Wananchi wanahimizwa kuwa na moyo wa uzalendo na zaidi kujivunia kuwa Wakenya kivitendo. Aidha, wanahimizwa kutambua uhalisia wa maisha (bila ya kujidharau) kuwa hakuna kinachomtosha au kutomridhisha mja. Kuendekeza tamaa ni kuwa mtumwa wa maisha na kwamba hilo ni jambo la kidhahania linalojenga walakini katika fikra au bongo za wananchi wasiokuwa na utu.

## Hitimisho

Zimwi la ufisadi katika taifa la Kenya lipo na linahitaji kutafutiwa tiba ya dharura. Katika nchi hii, mipasho na suluhu inaweza kupatikana (bila ya matumizi ya vitisho visivyofaa) kupitia kwa methali za Kiswahili ambazo ni kauli za asili. Sababu ni kwamba hizo ni kauli muhimu zinazotokana na utamaduni wa wenyeji. Mapambano dhidi ya ufisadi katika jamii na kwa mataifa yanayoendelea huwa safari ngumu na ndefu. Wananchi wa Kenya wanahitaji kujengewa mazingira ya kutambua kuwa ni wajibu wa kila mmoja kujitahidi kadri ya uwezo wake katika kuuondoa ufisadi. Ingawa kitumbua kimeingia mchanga; hakijaoza na kinaweza kusafishwa. Aidha, wananchi wa taifa hili wana jukumu (na ni wajibu wa kila mtu) kuiandama safari hii ya kusafisha, kufufua na kuirejesha sifa ya jina la Kenya katika ngazi ya umataifa. Ni katika mazingira haya ambapo wananchi watasanzua utandu uliowagubika na kuwalemaza. Ni katika hatua hii ambapo wananchi watashikana mikono kujivunia kuwa Wakenya kwa dhati. Jamii hii imekuwa ikitambaliwa na kuteseka kwa vitimbi vya ufisadi ambvyo vimekuwa vinaendelezwa kwa uwazi au chini kwa chini; siyo kutoka nje bali kutoka ndani. Hata hivyo, jamii kwa ujumla inahitaji kuzinduliwa na kubadili milekeo yake kuhusu dhana ya utajiri au kujipatia 'riziki' kwa njia ya ulaghai. Nguvu na vitisho vimekuwa vikitumiwa lakini pia busara ya methali inaweza kutoa uelekezi kwa wananchi. Methali za Kiswahili zimekuwepo na zipo ili kutumiwa katika harakati ya kuelekezana na kujengea mwafaka huo wa kuuondoa ufisadi nchini. Methali hizo zinaweza kutumiwa kubainisha na kukabiliana na nduli hii ya ufisadi kwa kuzingatia viwango viwili: cha mtu binafsi na umma kwa ujumla. Isitoshe, methali za Kiswahili zina lengo moja muhimu: kuwa mlinzi au mhifadhi wa haki katika jamii. Hili linahimizwa ili kuhakikisha kuwa, watu wanaishi kwa amani, upendo na umoja. Endapo methali hizi za Kiswahili zitamuktadhishwa ipasavyo, mwafaka huo utashuhudiwa katika nchi hii. Matokeo yatakuwa ni wananchi kurudisha matumaini na kupalilia ndoto ya wale waliopigania uhuru wa nchi hii. Isitoshe nchi hii haitasimama katua kama ghofu bali kama ngome au kivutio cha uwekezaji wa kiuchumi katika sayari hii. Hakuna haja ya wananchi kusususika kwa kuishilia kwa 'tungalijua' bali suala la ufisadi linahitaji kuhusishwa zidi katika mitaala ya shule; kuanzia viwango vya chekechea hadi vyuo vikuu.

**Marejeleo**

Abou-Zaid, A. S. (2013). 'The U.S. Folklore, Proverbs, and Economic Behavior' in *Economics & Sociology, Vol. 6, No 2, pp. 126-131.*

Babatunde, A. A. na O.S. Mujidat. (2014). 'The Place of Indigenous Proverbs in Peace Education in Nigeria: Implications for Social Studies Curriculum' in International Journal of Humanities and Social Science Vol. 4 No. 2 [Special Issue – January], uk. 186.

Hassan, A. (2016). 'Ufisadi ni zimwi linalotafuna jamii yetu,' katika *Taifa Leo, 5.2.2016, uk. 25.* Nairobi: Nation Media Group Ltd.

Kalugila, L. na A.Y Lodhi. (1980). *Methali zaidi za Kiswahili toka Afrika Mashariki.* Uppsala: Scandinavian Institute of African Studies.

Maitaria, J.N. (2014a). "Methali za Kiswahili katika kuelimishia kuhusu Uwiano na Utangamano wa Kitaifa" katika Simala, I; L. Chacha and M. Osore (wahr.) *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya.* Nairobi: Twaweza Communications, (pp.163-178).

Maitaria, J.N. (2014b). "Methali za Kiswahili kama Chombo cha Kusuluhishia Migogoro katika Jamii" katika Simala, I; L. Chacha and M. Osore (wahr.) *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya.* Nairobi: Twaweza Communications, (kur.133-149).

Maitaria, J.N. (2018). "Methali za Kiswahili kama Kitambulisho cha Utamaduni wa Mwafrika" in Ndungo, L.M., Ngugi, P.M.Y., Makokha, J.S & Ngugi, D (wahr.) *From Asmara 2000 to Nairobi 2014: Trends in African Languages and Literature.* Nairobi: Institute of African Studies, Kenyatta University.

Mbonde J.P. (2005). 'Methali za kiutandawazi.' Makala yayaliyowasilishwa katika Kongamano la Jubilei ya Miaka 75, tarehe 4 -7 Julai 2005 katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Mieder, W. (2008). *Proverbs Speak Louder than Words.* New York: Peter Lang Publishing, Inc.

Murithi, B.M.J. na Wanderi, K. (2016). 'Ufisadi Kenya waangaziwa kimataifa' katika gazeti la *Taifa Leo,* 14.5. 2016, uk. 3. Nairobi: Nation Media Group Ltd.

Mutuambo, A., Samuel, K. na Valentine, O. (2016) 'Jengo la orofa nne katika mtaa wa Zimmerman, Nairobi ambalo lilitiliwa shaka miaka miwili iliyopita liliporomomoka usiku kuamkia jana.' katika *Taifa Leo* 10. 3. 2016, *uk.* 2. Nairobi: Nation Media Group Ltd.

Nsokwa, J. (2011). 'Dokezo za ishara katika methali za Kiganda'. Kampala: Chuo Kikuu cha Makerere. Tasnifu ya Uzamifu. (Haijachapishwa)

Onyango,L. (2016). 'DUALE AMJIBU RAILA' katika *Taifa Leo,* 29. 2. 2016, kur. 1-2. Nairobi: Nation Media Group Ltd.

Wanjohi, G. J. (1997). *Under One Roof-The Gikuyu Proverbs; & The Wisdom andPhilosophy of African Proverbs: The GikuyuWorld-View.* Nairobi: Paulines Publications Africa.